## KANUNI ZA KILIMO BORA CHA CHOROKO

- Mbegu kwa ajili ya kupanda: Chagua mbegu zenye ubora unaokubalika, zilizopendekezwa na watafiti pamoja na kamati ya udhibiti ubora wa mbegu.

- Eneo linayofaa kwa zao la choroko: Chagua eneo lenye udongo usiotuwamisha maji, lisilo na mteremko mkali, lenye rutuba ya kutosha na lenye udongo wa kichanga.

- Maandalizi ya shamba: Andaa shamba mapema kwa kutifua udongo ili upitishe hewa ya oksijeni na maji kwa urahisi, lima magugu ili kuruhusu kukauka na kuoza vizuri.
- Tumia Jembe la mkono au la kukokotwa kwa ng'ombe hata hivyo trekta hufanya kazi kubwa na rahisi zaidi.

- Pia wasiliana na vituo chini ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) vilivyopo kila kanda kuhusiana na utaratibu wa kupima udongo ili kujua afya ya udongo wa shamba lako na hatimaye kujua kiasi na aina ya mbolea utakayotumia.

- Mbolea za kupandia: Kuna vyanzo mbalimbali vya kuboresha afya ya udongo kama vile Samadi, Mboji, Mbolea ya Kijani, Mbolea za viwandani na Masalia ya mazao. Aidha kilimo hifadhi na kilimo cha mzunguko huboresha afya ya udongo.

- Matumizi ya samadi: Tumia kiasi cha tani 24 za samadi kwa ekari, iwe iliyooza na kuhifadhiwa vizuri pasipo kuathiriwa na mvua au jua ama inapatikana, ichanganye kikamilifu kwenye shamba wakati wa kulima.

- Matumizi ya mbolea za chumvuchumvi: Hii inategemea na ,matokeo ya afya ya udongo kwa wakati huo. Japokuwa inashauriwa kutumia walau mfuko mmjoa wa mbolea ya DAP, TSP, NPK, au Minjigu mazao kulingana na matokeo ya hali ya afya ya udongo na mazao.

- Kwa ushauri zaidi wasiliana na mtaalamu wa kilimo aliyekaribu nawe au wasiliana na wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo kupitia anuani zifuatazo hapa chini.

**Mawasiliano kanda ya Kaskazini:**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
Kituo cha Utafiti Kilimo Selian
S.L.P 127, Selian
Simu/Nukushi: +255 736 500 538
Barua pepe: cdselian@tari.go.tz
Tovuti: www.tari.go.tz

**Mawasiliano kanda ya Mashariki:**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
Kituo cha Utafiti Kilimo Ilonga
S.L.P , 33 Kilosa, Morogoro
Simu/Nukushi: +255 736623283
Barua pepe: cdilonga@tari.go.tz
Tovuti: www.tari.go.tz

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA

TARI
Transforming Agriculture

# TUMIA MBEGU BORA ZA CHOROKO KUONGEZA TIJA NA KIPATO



**Kwa Mawasiliano:**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
Kituo cha Utafiti Kilimo Ilonga
S.L.P , 33 Kilosa, Morogoro
Simu/Nukushi: +255 736623283
Barua pepe: cdilonga@tari.go.tz
Tovuti: www.tari.go.tz

KALRO NARO WorldVeg

## UTANGULIZI


Choroko ni zao jamii ya mikunde, ni zao la chakula na biashara. Choroko hustawi katika udongo wa aina tofauti usiotuamisha maji. Hustawi zaidi kwenye ukanda wa chini na wa kati, yaani mita 0 hadi 1500 kutoka usawa wa bahari. Pia choroko ni zao linalostahimili ukame. Choroko hukomaa kwa siku 60 hadi 75 kulingana na aina. Choroko hazihitaji maji mengi hivyo hupandwa miezi miwili kabla ya kumalizika kwa mvua za masika, pia choroko huweza kupandwa kipindi cha mvua za muda mfupi (vuli). Mojawapo ya faida zake ni kama (i) Chanzo cha viini lishe kama protini, madini ya chuma na zinki kwa binadamu (ii) Chanzo cha kipato katika kaya na taifa kwa ujumla (iii) Kurutubisha udongo (iv) Usalama wa chakula.

**Aina za mbegu bora za chororoko Tanzania**

Taasisi ya utafiti wa kilimo Tanzania (TARI) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamegundua mbegu bora nne za choroko zenye sifa zifuatazo.

### 1. TARI -G- GRAM 1

- Mbegu bora iliyopitishwa na taasisi ya udhibiti ubora wa mbegu mwaka 2022
- Inakomaa mapema kati ya siku 62-71 katika ukanda wa chini na wa kati
- Insatahimili magonjwa ya aina ya kirusi na chule
- Uzao wake ni gunia 8 hadi 15 zenye ujazo wa kilo 100 kwenye hekta moja
- Inastawi maeneo yenye mvua za wastani
- Mbegu zake zina ukubwa wa wastani, zinang'aa zenye rangi ya kijani.



### 2. TARI -G-GRAM 2

- Mbegu bora iliyopitishwa na taasisi ya udhibiti ubora wa mbegu mwaka 2022
- Inakomaa mapema kati ya siku 64 - 75 katika ukanda wa chini na wa kati
- Inastahimili magonjwa ya aina ya kirusi na chule
- Uzao wake ni gunia 9 hadi 17 zenye ujazo wa kilo 100 kwenye hekta moja
- Inastawi maeneo yenye mvua za wastani
- Mbegu zake zina ukubwa wa wastani na hazing'ai.




### 3. NURU

- Mbegu bora iliyopitishwa na taasisi ya udhibiti ubora wa mbegu mwaka 1980s'
- Inakomaa mapema kati ya siku 55 - 65 katika ukanda wa chini na wa kati
- Uzao wake ni gunia 7 hadi 15 zenye ujazo wa kilo 100 kwenye hekta moja
- Inastawi maeneo yenye mvua za wastani Mbegu zake zinang'aa.



### 4. IMARA

- Mbegu bora iliyopitishwa na taasisi ya udhibiti ubora wa mbegu mwaka 1980s'
- Inakomaa mapema kati ya siku 60 -65 katika ukanda wa chini na wa kati
- Uzao wake ni gunia 8 hadi 15 zenye ujazo wa kilo 100 kwenye hekta moja
- Inastawi maeneo yenye mvua za wastani Mbegu zake zina rangi ya kijani na hazing'ai.



## NAFASI YA KUPANDA

Panda umbali wa sentimeta 50 msitari hadi msitari na sentimita 10 shina hadi shina na mmea mmoja kwa shimo au sentimenta 20 shina hadi shina na mimea miwili kwa shimo.

## UDHIBITI WA WADUDU

Zuia wadudu kwa kupulizia kiuadudu kimojawapo kati ya karate, amerate, profecron au kingine utakachoshauriwa na wataalamu wa kilimo. Zingatia ushauri utakaopewa kwa kutumia viuatilifu vili-yopendekezwa na uzingatie maelezo yaliyoko kwenye kifungashio cha kiuatilifu hicho.

## PALIZI

Hakikisha shamba linakuwa safi wakati wote ili mimea ikue katika hali ya afya na kusaidia kuongeza mavuno. Tumia kiuagugu kuzingatia ushauri wa wa-taalam na pia palizi ya jemebe la mkono kulingana na magugu yaliyoota shambani

## KUVUNA NA KUHIFADHI

Choroko zivunwe wakati zimekauka vizuri kabla ya vitumba kuanza kupasuka ili kuzuia upotevu wa mazao shambani.

CamScanner